**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**650** **HAIBA NA MICHEZO**

**Muda: Saa 3.** **Mwaka : 2016**

---

**MAELEKEZO.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka sehemu **B**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na sehemu **B** ina alama **sitini (60)**.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (40 Alama)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii

1. Eleza uhusiano uliopo kati ya kitabu cha kiongozi cha mwalimu na muhtasari wa somo.

2. Taja mambo manne yanayopaswa kuzingatiwa na mwalimu kabla ya kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia.

3. Eleza sababu nne za kufanya uchambuzi wa kiongozi cha mwalimu wakati wa maandalizi ya somo.

4. Fafanua aina nne za maswali yanayoweza kutumika kupima maendeleo ya wanafunzi katika somo la Haiba na Michezo.

5. Toa maana ya dhana zifuatazo kama zinavyotumika katika somo la Haiba na Michezo:

    (a) kufaragua
    (b) zana mpitisho
    (c) zana mafunzo
    (d) zana za kujifunzia.

6. Eleza kwa kifupi maana ya istilahi zifuatazo kama zinavyotumika katika andalio la somo:

    (a) ujuzi
    (b) lengo kuu
    (c) mada ndogo
    (d) lengo mahsusi.

7. Toa hoja nne kuonesha uhusiano uliopo kati ya azimio la kazi na andalio la somo.

8. Taja misingi minne ya ufundishaji wa somo la Haiba na Michezo.

9. Eleza sababu nne zinazoweza kusababisha usalama wa wachezaji kuwa hatarini wanaposhiriki michezo.

10. Bainisha stadi nne za maisha ambazo mwanafunzi anajengewa kwa kusoma somo la Haiba na Michezo.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU B (60 Alama)**

Jibu maswali manne tu katika sehemu hii

11. Eleza maandalizi ya maandiko, vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia kwa somo la Haiba na Michezo.

12. Changanua umuhimu wa upimaji na tathmini katika ufundishaji wa somo la Haiba na Michezo.

13. Jadili nafasi ya zana za kufundishia na kujifunzia katika kufanikisha mchakato wa ujifunzaji.

14. Eleza hatua zinazopaswa kufuatwa na mwalimu katika maandalizi ya ufundishaji wa somo la Haiba na Michezo.

15. Tathmini changamoto zinazojitokeza wakati wa maandalizi na matumizi ya zana za kufundishia na kujifunzia.

16. Eleza kwa kina misingi ya ufundishaji wa somo la Haiba na Michezo na jinsi inavyomsaidia mwalimu kufanikisha somo.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org